

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu: 202-884-1080
202-939-6125
Nukushi: 202-797-7408
Barua pepe: ubalozi@tanzaniaembassy-us.org

1232 22nd Street, N.W.,
WASHINGTON, D.C. 20037

Kumb. Na. KBA 195/655/01/'C'/'

15 Disemba 2016.

Wenyeviti/Makatibu,
Jumuiya za Watanzania (Diaspora)

YAH: UFAFANUZI WA SHERIA YA ARDHI KWA DIASPORA MTANZANIA.

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Ubalozi umepokea ufafanuzi wa Sheria na Haki za Umiliki wa Ardhi kwa raia wa Kitanzania na yule aliyeukana uraia. Ufafanuzi huo ni kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Tunaomba kunukuu ufafanuzi huo kama ifuatavyo:

“Kwa mujibu wa **Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995, chini ya fungu la 7(2)**, mtu yoyote ambaye ni Mtanzania akichukua uraia wan chi nyingine, mtu huyo atakoma kuwa Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”

Aidha, Sheria nyingine inaeleza kuw **“Fungu la 19 na 20 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999**, raia yoyote wa kigeni haruhusiwi kumiliki ardhi Tanzania isipokuwa kwa ajili ya uwekezaji na atapewa Hati isiyo asili (Derivative Right) kupitia Kituo cha Uwekezaji”.

Vile vile, Wizara ya Ardhi imefafanua kuwa Sheria hizo mbili tajwa hapo juu, zina maana kuwa “Mtanzania ambaye ameukana uraia wake, kwa kuwa anakoma kuwa Raia wa Tanzania, Sheria hiyo inamnyima fursa za kumilikishwa ardhi”.

Tunatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano wenu na tunawatakia kazi njema.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'D.A.' or similar initials.

Dismas A. Assenga,
kny. **BALOZI**